
# KUGIE UTHERI

## NDUMIRIRI YA IBUKU RIA NGAI



# KUGIE UTHERI

Mwandiki: Paula Kirkpatrick na Joan Carter

Mathomo ma micemanio ya Atumia

Africa Coordinated Curriculum for Women

Co-Lit 2-2-1

Published and Printed by
Baptist Publication House
Box 30370, Thika Road, Nairobi

© Copyright, 1990

Baptist Publications House

All rights reserved

kuhunjia na kumaruta. Atumia Abatisti nimari nguo yao ya bururi ya rangi wa puple na mweru. Nigetha mutumia etikirio kumikira no nginya erute mihari ya kirikaniro ya kumuteithia kuhunjiria aria angi uhoro wa uhonokio.

**GICUNJI GIA KERI:** Gutumira kirikaniro

Miaka mirongo iri na itano nithiru Zambia kwari amiceni atano tu na atumia ao. Makanitha na atungatiri mari anini. Amiceni magitua cira ati mathomo ma kirikaniro na njira ya posta no mateithie kwira aria angi uhoro wa Jesu.

Ibuku ria mbmere riari ;"Jesu Nuu? Mabuku mangi kenda nimandike niundu wa mubango uyu wa mathomo ma kirikaniro na njira ya Posta. Mabuku maya mandikitwo na ruthiomi rwa; Githungu, Chichewa, Bemba na kaonde. Mabururi mangi mirongo iri na umwe riu mari na mubango ucio wa mathomo(Bible Way Correspondence School).

O mweri arutwo nimeyandikithagia na magetikia Jesu. Makanitha maingi mambiriirio ni arutwo aya.

**GICUNJI GIA GATATU:** Kurutana

Kahinda ka miaka mirongo ina Moses Chimfumpa athiite kuraya na Ngai. Riu ni mutongoria wa Abatisti

Ari na miaka 43 nietikire mwito wa Ngai gutuika ndungata ya wira wa wake na agithii Seminary ya Zambia. Thutha wa kurikia agituika mutungatiri na akihingura makanitha maingi. Thutha akiruta wira na kiama kia "Mathomao ma Kirikaniro na Njira ya Post." Agicoka aagituika mwarimu wa Seminary.

Mathomo maria Moses athomire matumire aguciririe andu aingi kuri Kristo.

**GICUNJI GIA KANA:** Kurima

Abatisti a Zambia maheirwo mugunda wa ika 2,088. Wammbiriirio ni Dr. Moffat, wa muhiriga wa a David Livingstone. Riria akuuire andu ao makiuheana kuri abatisti.

Mkumiceni umwe aikaraga kuo na agateithia kuruta aneu a Zambia urimi na kuriithia mahiu. Kuri uhandi wa ngano, urithi wa nguku, na uriithi wa ng'ombe na ndegwa cia nyama. Kanitha na cukuru ya atungatiri iri o kuu.

**MUTONGORIA:**

Andu othe Zambia marutithanagia wira hamwe. Riu kuri na wiyathi wa kuhunjia. Rekei tumahoere nigetha Ngai amateithie kurugama wega.



## MAUNDU MARIA MARI-HO

## NDUMIRIRI YA KIRIKANIRO KURI ANDU OTHE

Mwandiki: Paula Kirkpatrick


1. Mubango wa Ngai
2. Ngai agithura Iburahimu
3. Musa agitongoria Andu a Ngai
4. Aria Angi Marumiriire Ngai
5. Mubango wa Ngai kuguuririo Kuri Anabii
6. Jesu Kuhingia Mubango wa Ngai
7. Jesu na Ayahundi
8. Jesu na Andu a Nduriri iria Ingi
9. Gukua na Kuriuka Kwa Jesu
10. Urutani wa Jesu wa Muthia
11. Roho Mutheru Aheanaga Hinya wa Kuhunjiria Andu
12. Zambia: Riu Mundu No Ahunjie
    Mwandiki: Joan Carter


Co-Lit 2-2-1

**MUTONGORIA:**

Mubango wa Ngai nduri wagaruruka. No mubango wa Ngai wari andu othe mamumenye we ta Ngai Umwe na wagutio. Kuma riria Jesu ari guku thi andu ake metagwo Akristiano. Mathuritwo kuhingia kirikaniro giake. Uria wothe wamukirite Jesu ari na murigo wa kumenyithia aria angi wendo wa Ngai thi yothe o ta uria ciana cia Iburahimu ciari naguo.

Mubango wa Ikumi na Igiri

## ZAMBIA RIU MUNDU NO AHUNJIE

**Muoroto wa Ithóma:** Umiceni

**Maandiko Matheru:** Atumwo 28

**Muhari wa Kwiririkania:**

"Akamahunjiria uhoro wa uthamaki wa iguru, akamarutaga maundu ma mwathani Jesu Kristo omiriirie muno, hatari mundu ungimugiria" Atumwo 28:31

**MUTONGORIA:**

Hindi riria Paulo ari thiini wa njera ari na wiyathi kuhunjia. O nagukorwo ari muohe na minyororo niangierire thigari na ageni ake uhoro w auhonokio wa Kristo. Muhari witu wa kwiririkania niguo utwirite (Taucokere!)

Muhari ucio wina kionereria kia Abatisti a Zambia umuthi. Atungatiri na amiceni riu mari wiyathi kuhunjia na kurutana. Reke twirute uria mekaga.

**GICUNJI KIA MBERE:** Kuruta Wira Hamwe

Abatisti a Zambia na amiceni ni aigite muoroto wa kuhota gukinyira andu millioni 7.1 cia bururi wa Zambia. makanitha nimandikaniire na makarikanira magwatanire. Metikaniriirie hamwe kurutaga gicunji kinini kuma kuri muhothi wao niundu w aguteithia amiceni a konibeniconi yao na kuriha arimu eri a Seminary yao. mwaka wa 1994 nimuoroto kuriha andu aya hamwe na mawira mangi mao.

Mari na njira nyingi cia gukinyira andu na kiugo. Na njira ya Radio; iria iri na ibindi inya cia thiomi mwanya mwanya. Mabuku ma sunday school na ma atumia.

Na iguru ria mkothe aatkumia a Zambia marutithanagia wira hamwe na makanitha hari mubango wa

## Roho Mutheru Aheanaga Hinya Wa Kuhunjiria Andu

**Muoroto wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Atumwo 2:1-12;38-39

**Muhari Wa Kwiririkania:**

"No ni muriheo hinya, Roho Mutheru aarikia gukinya iguru rianyu: na Mutuike aira akwa o Jerusalemu na Judea guothe, na Samaria, o na kinya ituri ciothe cia thi". Atumwo 1:8

**MUTONGORIA:**

Thoma ringi Atumwo 2:1-12,38-39. Mihari ino itwiraga gitumi na ihinda riria Roho Mutheru okire.

Thutha wa atumwo kwamukira hinya wa Roho Mutheru, ni mehariirie kuhingia mubango wa Ngai wa kurehe andu a iruka ciothe kuri Ngai. Naundu wa hinya wa Roho Mutheru gakundi kanini gagitwara uhoro mwega kuri andu othe athi.

**GICUNJI KIA MBERE:** Ayahundi Makiigua Uhoro Mwega Muthenya wa Pentekosti

Kionereria kimwe gia guka kwaRoho Mutheru muthenya wa Pentekosti ni atumwo kuheo uhoti wa kwaria na thiomi ikumi na ithano. Mahunjirie o mundu wothe wokite iruga-ini riu ria Pentekosti, o mundu na ruthiomi rwake akiigua ndumiriri.

Hindi iria Petero ahunjiirie andu makiria ya ngiri ithatu magitua cira kurumirira Jesu Muthenya ucio wa Pentekosti.

**GICUNJI GIA KERI:** Andu a Nduriri Ingi Kuigua Uhoro Mwega

Thoma Atumwo 10:21-33. Thiini wa mihari ino kuri na rugano rwa mundu wa nduriri. Korinelio ari munene wa thigari igana cia Aroma. Ndari muyahundi no ari mundu wahoyaga Ngai. Petero niarumiriire mutaratara wa Ngai gutwarira koronelio uhoro mwega. Thoma Atumwo 10:34-35. Ngai ekaga andu othe maundu maiganaine.

**GICUNJI GIA GATATU:** Thi yothe Kuigua Uhoro Mwega

Thoma Mathayo 28:19-20. Roho Mutheru atongoririe ahonoki a mbere kuri icigo ciothe cia thi. Mathiaga makiraga andu othe kundu guothe mathiaga uhoro wa Jesu na gukua gwake na kuriukio. Andu aingi magitikia. Etikia maikarire mari ehokeku kuri Jesu ihinda ria minyamaro miingi. Thoma Atumwo 5:41-12.





## MUBANGO WA NGAI

**Muoroto wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Aefeso 3:1-3

**Muhari Wa Kwiririkania:**

"No riri, undu uria ngai onanitie utwendi wake naguo-ri, ni uyu, ati Kristo atukuiriire riria twatuire turi o ehia." Aroma 5:8

**MUTONGORIA:**

Thoma Kiambiriria 1:1. Kirikaniro kiugaga ati Ngai ombire iguru na thi. Na gigacoka gigatwira kiria giatumire ombe thi.

No wirute mubango wa ngai kuri andu othe na waku na njira ya guthoma Kirikaniro.

**GICUNJI KIA MBERE:** Bata wa mubango

Icunji ikumi na kimwe cia mbere cia ibuku ria kiambariria gitwiraga uhoro wigie umbi wa thi na mundu. Matuku-ini ma kirikaniro gikuru Ngai aguuririe mubango wake kuri arathi na andu aria mari atheru. Thiini wa kirikaniro kieru Ngai aguuririe mubango wake kuhitukira kuri muriu wake Jesu Kristo.

**GICUNJI GIA KERI:** Kuguurio Kwa Mubango

Jesu niwe waguurire mubango wa Ngai kuri mundu. Riria Jesu okire na agikua mutharaba-ini ninduwa mehia maitu, nionanirie

Uria wendo wake utarii. Thoma Aroma 6:8

**GICUNJI GIA GATATU:** Mubango kugaywo

Mawira mothe ma uhonokio wa mundu wathirire riria Jesu akuire mutharaba-ini na akiriuka kuma mbirira-ini na akiambata iguru. Andu othe riu no moke kuri Ngai, na njira ya witikio niundu wa wega wa Ngai. Thoma Aefeso 2:8.

**MUTONGORIA:**

Thoma Johana 14:6. Mubango wa Ngai ni ati mundu ature na ngwataniro na Ngai kuhitukira thiini wa muriu Jesu Kristo.

# NGAI AGITHURA IBURAHIMU

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Atumwo 7:2-8

**Muhari Wa Kwiririkania:**
**"Nake akiihoka Jehova; naguo undu ucio Jehova akimutuira ta ari uthingu e naguo"** Kiambiririia 15:6

**MUTONGORIA:**
Thutha wa mundu kwihia agituika mwaganu muno. Mehia magithukia ngwatiniro ya mundu na Ngai.

No Ngai akiambiriria mubango wa gucokia ngwataniro yao na mundu.

**GICUNJI KIA MBERE:** Kwirirwo kwa Iburahimu

Ngai ambiririe mubango wake na gucagura mundu wetago Iburahimu. Ndamucagurire niundu wa uthingu wake, no niundu wa gwathikira Ngai. Ngai akimwira athame mucii wake na athii bururi ungi. Na agiathika. Niundu wa gwathika Ngai niahotire gutumira Iburahimu thiini wa mubango wake. Thoma kiambiririia 12:1-3.

**GICUNJI GIA KERI:** Kwirirwo kwa Isaaka

Ngai agererie wathiki wa Iburahimu na kumwira arute mwana wake wa mumwe,Isaaka, ta igongona. Agiathika nake Ngai akumunengera ndurume ya igongona. Iburahimu nietikitie Ngai ati o na muriu Isaaka akua niakumuriukia. Thoma Ahimbirania 11:19

Isaaka atuuika mundu mugima, Ngai agicokera kirikaniro giake kuri we. Thoma Kiambiririia 2:5

**GICUNJI GIA GATATU:** Kirikaniro kuri Jakubu

Jakubu ari umwe wa mahatha ma Isaaka. Ritwa riake riugaga "muhenania." Ahenirie muru-wa-nyina Esau na akimutunya urigithathi. Na kwauguo akimuheneria uhoro wake wa kuoya kirathimo kuma kuri ithe Isaaka.

Hindi irira Jakubu oraga kuma kuri marakara ma muru-wa-nyina Esau ,Ngai akiariria Jakubu thiini wa kiroto. Jakubu akiambiririia kwiruta kuma kuri Ngai. Akiiruta ati Ngai ni Ngai wa andu othe.

Ritwa riake kahinda ka miaka miingi niriacenjirio kuma Jakubu na agituika Isiraeli riria riugaga"Uria ugianite na Ngai"(Thoma Kiambiririia 35:16)

**MUTONGORIA:** Iburahimu, Isaaka, na Jakubu mari andu a witikio. Nimetikitie Ngai na makiruta kumwathikira. Hitho ya kuona irikanirio cia Ngai ihingite ni gwathikira Ngai.





# URUTANI WA JESU WA MUTHIA

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Atumwo 1:1-11

**Muhari wa Kwiririkania:**

"Jesu agikimera ringi atiri, giai na thayu ota uria ithe witu aandekirie nii, noguo ndamurekia inyui". Johana 20:21

**MUTONGORIA:**

Thutha wa Jesu kuriukio kuma kuri akuu, niaumiriire atumwo ake maita maingi ihinda riu ria thiku mirongo ina, atanambata iguru. Jesu niaririkanirie atumwo ake hakuhi maita matano thutha wa kuriuka ati niio magatuara uhoro mwega thi yothe.

**GICUNJI KIA MBERE:** Urathi wa Ngai Kuhinga

Thoma Luka 24:44-47. Hwaini wa muthenya uria ariukire, Jesu niaumiriire atumwo ake ikumi na aria macemanitie hamwe nao. Jesu akimera ati urathi wothe wa Kirikaniro Gikukru umukonii ati niwahinga. O hindi iyo Jesu akihingura meciria ma atumwo ake magitaukirwo ni Maandiko maria mathomete. Thoma Luka 24:25.

**GICUNJI GIA KERI:** Jesu Akiumirira Arutwo ake

Thoma Johana 20: 19-23,Johana 21:15-17. Thiini wa Johana 20:19-23,Jesu erire atumwo ake,"... o ta uria ithe witu aandekirie nii, noguo ndamurekia inyui".

Jesu atumaga atumwo ake thi yothe na wira wagwika. Amatumirena ndumiriri yake ya wiriri na uhonokio wa thi yothe. Thutha ucio akimahe hinya wa Roho Mutheru wa kumatongoragia kurutawira wake.

Thiini wa Johana 21:15-17, Jesu ariirie Petero uhoro wa uritu wa murigo wake thiini wa uthamaki wa Ngai.

**GICUNJI GIA GATATU:** Riathani Inene Ria Jesu

Thoma mathayo 28:16-20. Jesu erire atumwo ake matware ndumiriri yake thi yothe magitumaga andu othe matuike arumiriri ake. To kumatha amathire no niamerire ari hamwe nao hindi ciothe magithii kinya ithiriro ria uturo.

**MUTONGORIA:**

Thiini wa Maandiko macio Jesu aarera atumwo ati nio magatwara ndumiriri yake ya uhonokio thi yothe. Na niamerire ati matigakorwo mari oiki. Amerire agakorwo ari nao kundu guothe magithii makiraga andu uhoro wa Jesu.

# GUKUA NA KURIUKA KWA JESU

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Mariko 15:21-39

**Muhari wa Kwiririkania:**

"Nake Jesu akimera atiri, Ni nii njira, na ni nii uhoro-wa-ma, na ni nii Muoyo; gutiri mundu ukinyaga gwi ithe witu, atokiire hari nii." Johana 14:6

**MUTONGORIA:**

Ritwa Kristo ni kiugo gia kiyunani kiugaga Muhonokia na Kiihibirania. Muhonokia na Kristo ciugaga muitiririe maguta. Athinjiri Ngai, Anabii,na athamaki othe nimaitagiririo maguta. Jesu ari muthinjiri-Ngai, Munabii, na Muthamaki. Na ningi ari gaturume ka Ngai ga guthambia mehia ma kirindi gia thi.

**GICUNJI KIA MBERE:** Kwiruta ta Igongona Mutharaba-ini

Thoma Ahibirania 9:28; 1 Johana 2:2. Jesu erutire ta Igongona

tondu gutiari na njira ingi ya uhonokio gukinyira andu othe. Naaundu wa gikuu giake nitutuitwo akinyaniru a kugaya uthamaki wa Ngai. Tugagituo ciana cia Ngai naundu wa thakame iria aitire. Thoma Johana 1:12.

**GICUNJI GIA KERI:** Muturire Mueru Thiini wa Kristo

Immanuel ni mundu muithi wa bururi wa Nigeria. Atungatiire ngoma na hinya wake wothe. O na niangiaraniirie na shaitani ta uria mundu aragia na uria ungi. Niahuthagirwo ni shaitani kunyarira ahonoki.

No hindi iria agomanire na hinya wa thakame ya Jesu, agikuruo biu kuma minyororo-ini ya shaitani. Riu andikite uira wake thiini wa ibuku riake ritagwo "Gukuruo kuma Mahinya-ini ma Nduma" (Delivered from the power of Darkness)

Immanueli riu nikiumbe kieru. Ena muturire mueru. Ithuothe noturute uira wa muturire mueru thutha wa kwamukira Kristo.

**MUTONGORIA:**

Undu umwe wa goro muno thiini wa rugano rwa thi ni gikuu na kuriuka kwa Jesu. Mutharaba-ini iguru Jesu agiithirania undu urua mundu atangiahorire ari we. Hindi iria Ngai ariukiirie Jesu kuma kuri akuu, gukihoteka ati andu othe matuike gicunji kia mubango wa Ngai.





# MUSA AGITONGORIA ANDU A NGAI

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Atumwo 7:17-34

**Muhari wa Kwiririkania:**

"Riiu-ri witikio niguo umenyithagia ati maundu maria merigiriirwo ni ma ma, na niguo wi kihooto gia kumenyithania ati maundu maria matonekaga mari ho. Amu-ri, ni undu waguo athuri aria a tene nimaagiire na ngumo njega". Ahibirania 11:1-2

**MUTONGORIA:**

Miaka iria ciana cia Isiraeli ciaturaga misiri, gicunji kia mbere gia kirikakniro kia Ngai kuri Iburahimu gikihinga, makiongerereka na namba. O na kinya kuherithio-ini kunene kuma kuri andu a Misiri, Aisiraeli magithii na mbere kuongerereka na namba na kugia na hinya. Ngai agicagura mundu wetagwo Musa atongorie ciana cia Isiraeli mathii bururi wa kirikaniro na mathondeka bururi wao..

**GICUNJIJI KIA MBERE:** Utongata wendaga waathiki

Ihinda ria mieri itatu thutha wa ciana cia Isiraeli kuma Misiri Ngai akimariria kirima-ini gia Sinai....... Mbere Ngai arririe Musa. Akimerira kkkkkumarathima maiga mathani make. Thoma Kiambiriria 19:5-6

**GICUNJI GIA KERI:** Aisiraeli Nimaregire Gwitikia Kirikaniro Kia Ngai

Rugano rwa ciana cia Isiraeli ni rwa kieha muno. Ngai erire ciana cia Isiraeli mathii maingire bururi wa kirikaniro. Makirega. Matietikirie Ngai.

Thoma Ndari 14:13-19. Musa niathaithire Ngai thutha wa andu aya kuhugukira Ngai hamwe nake. Aisiraeli maturire weru-ini ihinda ria miaka mirongo ina kinya riria Ngai arugamirie ruciaro rueru kuma.

**MUTONGORIA:**

Andu a Isiraeli matiataukiirwo no mubango wa Ngai. Matiathikiire Ngai na njira njiganu ya gutuma amehoke kumatumira guteitia aandu a nduriri iria ingi guthathaiya Jehova. Meciragia Ngai niwao oiki.

## ARIA ANGI MARUMIRIIRE NGAI

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Thaburi 67

**Muhari wa Kwiririkania:**

"Tondu ucio o na inyui endagai andu a kungi; ni undu ona inyui nimwatuire bururi wa Misiri muri andu a kungi" Gucokerithia Mathani 10:19

**MUTONGORIA:**

Thiini wa Kirikaniro Gikuru nituthomaga uhoro wa andu anduriri ingi, matari Aisiraeli merutite kuhoya Ngai. Andu a nduriri ingi nimetikagirio kuhoya Ngai meyunga na ayahundi. Thiini wa Kirikaniro Gikuru nituonaga andu aingi a nduriri ahoi Ngai mahinda mianya mianya.

**GICUNJI KIA MBERE:** Amwe Mathurire Ngai

Jethro ari muthoniwe wa Musa. Ari Mumindiani. Jethro akire kigongona na akihoya Ngai. Musa niagwatire Hobau ugeni, muriu wa Jethro, mathii rugendo na ciana cia Isiraeli nigetha agaye irathimo cia Ngai.

Balaamu, (Ndari 22), ndari Muhimbirania no ari murathi wa ndeto cia

Ngai. Hindi iria ciana cia Isiraeli ciambiriirie kuhota nduriri iria ingi na kuingira bururi wa kirikaniro mateithirio ni Rahabu. Akiamukira Jehova ta Ngai wake na Aisiraeli makimwamukira hamwe na andu a nyumba yake.

**GICUNJI GIA KERI:** Ruthu, Muoabi

Rugano rwa 'Ruthu ruonanagia ati Ngai niari na mubango na andu a nduriri irira ingi magie na gicunji hari mubango wake wa kurehe andu othe kuri we. Thoma Ruthu 1:1-18

**GICUNJI GIA GATATU:** Naamani Musuriata

Naamani ari munene wa mbutu cia ita cia muthamaki wa bururi wa Suriata. kuhitukira hari miiritu wa wira wa nyumba yao, Naamani niamenyire uhoro wa uhoro wa mundu wa Ngai wa Isiraeli. Na aagithii Isiraeli na akihonio murimu wa mangu. Kuma hindi iyo Naamani akiambiririra guthathaiya Ngai uria wa ma. Thoma 2 Athamaki 5:1-15

**GICUNJI GIA KANA:** Kiama Gia thi Kia Abatisti

Giki ni kiama gia makanitha mothe ma thi yothe ma kibatisti (Baptist world Alliance). Gikoragwo kiri na andu a mabururi mothe ma thi, nduriri na kabira ciothe cia thi yothe. Ni mubango wa Ngai ndumiriri ya Jesu Kristo ikinyire andu a mabururi mothe na kabira ciothe.





## JESU NA ANDU A NDURIRI IRIA INGI

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Johana 12:20-32

**Muhari wa Kwiririkania:**

"Amu uhoro wa guthurania Muyahundi na Muyunani gutiri: ni gukorwo Mwathani o ro ucio nowe Mwathani wa andu othe, na aikaraga o agitanahagira othe aria mamukayagira. Ni undu ni haandike atiri,mundu o wothe,ugakaira riitwa ria Mwathani ni akahonoka." Aroma 10:12-13

**MUTONGORIA:** Aisiraeli marega Jesu agithii kuri andu-a-nduriri iria ingi. Kirikaniro gitwiraga kundu kuingi uria kwahanaga hindi iria Jesu angiacemanirie na aria mataari Aisiraeli.

**GICUNJI KIA MBERE:** Jesu na Mutumia Mukaanani

Thoma Mathayo 15:22-28. Thiini wa rugano ruru Jesu ariirie mutumia uria wendaga ahonie mwari. Jesu akiamba kugeria witikio wa mutumia ucio na kumukirira. Na agicoka akimugeria na kumwira ati uhonokio wari wa Aisiraeli. No mutumia agithii na mbere na kumuthaitha. Gukuonania witikio uria ari naguo thiini wa Jesu. Naundu wa witikio wake mwari wake akihonio ni Jesu.

**GICUNJI GIA KERI:** Jesu na Munene wa Thigari Igana

Thoma Mathayo 8:5-13. Thiini wa rugano ruru Jesu ari Kaperinaumu hindi iria munene wa mbutu ya thigari cia Aroma amuririe athii na ahonie ndungata yake. Hindi iria Jesu etikirire guthii, mundu uyu Muroma akiuga atiri," Mwathani ndiagiriire ati utonye nyumba yakwa: no kiuge kiugo, na ndungaata yakwa niikuhona." (Aroma 8:8).

Jesu akigegio muno ni witikio wa mundu ucio. Na akira gikundi kia andu ati andu a nduriri aria mahana ta mundu ucio makauma thi yothe namaaagaikara thi thiini wa uthamaki wa Ngai hamwe na Iburahimu, Isaaka, na Jakubu.

**GICUNJI GIA GATATU:** Jesu na Mutumia Musamaria

Thoma Johana 4:7-26. Jesu niaunire mitugo miingi ya unduire ya Aisiraeli hindi iria aririe na mutumia Musamaria.

Jesu akira mutumia ucio ati matuku nimaroka maria andu makahoya Ngai na Roho na Ma. Jesu nietikirire kuri Musamaria ati niwe wari muhonokia uria weraniirwo ni Ngai na tunua twa anabii.

**MUTONGORIA:** Jesu arutire arutwo ake na umuthi araturuta na njira ya muturire wake. Jesu arutire atumwo ake na akimatuma nja ta aira ake. Mbere matumirwo kuri andu ao na thutha kuri andu othe a thi.

**GICUNJI KIA MBERE:** Musamaria Mwega

Thoma Luka 10;25-37. Thiini wa rugano ruru andu a ndini nimaremirwo ni guteithia mundu wa muhiriga wao. Nimwithiiri wa ruruka rungi, ruria rwamenetwo ni Aisiraeli muno, wateithirie mundu uyu watihangitio. Jesu akiuga tuthii na tutuike ta Musamaria uyu mwega. Jesu akiuga mundu abataire kuonania ati ni murumiriri wa waatho wa Ngai na ciiko no ti uria angiuga na kanua ati we ni mwitikia.

**GICUNJI GIA KERI:** Ngai Niaracaria Aria Morite

Thoma Luka 15:3-32. Rugano rwa thendi iria yorite, mburi iria yorite, na mwana uria worite; rutumenyithagia ati Ngai niaretha aria matamui. Nigukoragwo na kugoca kunene umwe urite oneka.

Thiini warugano rwa mwana uria worite, ithe ni Ngai. Muru- wa-nyina oyaga handu ha Aisiraeli. Kimwana giki kinini kionanagia andu-a-nduriri ingi; ithui twari kuraya muno na wendo wa Ngai. No na undu wa gwitikia thakame ya Jesu iria yaitirwo ithambie mehia maitu,tugagituika ciana cia Ngai. Muru-wa-nyina niaregire gukena muru wa nyina acoka. Uguo noguo ciana cia Isiraeli itakenirio ni gwitikia kwa nduriri iria ingi.

**GICUNJI GIA GATATU:** Iruga inene

Thoma Luka 14:16-24. Thiini wa rugano ruru mwathi ni Ngai na aria metitwo iruga ni Aisiraeli. No makirega na kwauguo Ngai agigita nduriri iria ingi cia thi, miingire iruga-ini. Ngai niareta mundu wothe thiini wa athi yothe aingire uthamaki-ini naundu wa kwamukira Kristo, ta muhonokia.

**MUTONGORIA:**

Atongoria aingi a ndini matietikitie ati Jesu ari muhonokia. Metireire muhonokia uria ungimakura kuma kuri wathani wa Aroma.

Hindi iria amerire matiitikitie makienda kumuraga.



**MUTONGORIA:**

Thaburi 67 yaragia uhoro wa gwituo kwa Ayahundi matware wega wa Ngai kuri nduriri ciothe cia thi. No makiremwo. Na nikio thiini wakirikaniro gikuru tuonaga turugano tunini tu twa andu a nduriri ingi matuikite andu a kuhoya Ngai uria wa ma.

Mubango wa Gatandatu

## MUBANGO WA NGAI KUGUURIO KURI ANABII

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Isaia 11:1-10

**Muhari wa kwiririkania:**

"Ni gukoruo thi niikaiyuruo ni uhoro wa kumenya riri wa Jehova; o ta uria mai miyuraga iria-ini makarihuba". Habakuku 2:14

**MUTONGORIA:**

Anabii a kirikaniro gikuru mariirie ciana cia Isiraeli uhoro wa mehia thiini wa muturire wa andu. Maheanaga ndumiriri ya kuringana na ihinda na muikarire wa andu acio.

**GICUNJI KIA MBERE:** Isaia

Ndumiriri ya Isaia yaugaga uhoro wa guka kwa muhonokia na uria mubango wa Ngai ugakinyanira. Thoma Isaia 7:10-25. Maandiko ma Isaia maritie uhoro wa ucio gukira anabii aria angi othe. Thiini wa Isaia 66, Isaia akiona kioneki kia mahinda maria nduriri ciothe igacaokanirira ithathaiye Ngai uria wa ma.

**GICUNJI GIA KERI:** Jonah

Thoma Jonah 1:1-17; 3:2-4;4:2-3. Ngai etire Jonah athii akahunjie bururi wa Nineve. Hindi iria Jonah ageragia kurira Jehova, akiiruta ati Jehova ni Ngai wa thi yothe.

Jona ndakenire hindi iria andu a Nineve meririre na makiambiriria kuhoya Ngai. Kuma kuri Jona Ngai akiruta aria etii a isiraeli ati we ni Ngai wa andu othe na ciumbe ciothe.

**GICUNJI GIA GATATU:** Malaki

Malaki ari munabii wa muthia uria Ngai athurite akanie andu ake athure. Andu a Isiraeli matiataukagirwo ni mubango wa Ngai kuri andu othe na kwauguo akimaririkania. Thoma Malaki 1:5.

Andu aria amure a Ngai nomamurakaragia. Thoma Malaki 1:10-11.

**MUTONGORIA:**

Kirikaniro gikuru githirite na gukanio na ritana ria wiriri kuriciana cia Isiraeli. Miaka magana maingi nimihituku kuma Ngai athondeka kirikaniro kiu na Iburahimu na bururi ugithondekwo rungu rwa utongoria wa Musa. O na gukorwo ciana cia Isiraeli itiataukagirwo ni mubango wa Ngai kuri bururi ucio,na kwauguo matiahotire gutwarithia mubango ucio.

Thutha wa miaka maagana maingi Ngai niangiahingire ndumiriri yake na kuhitukira kuri mwana wake Jesu Kristo, Ngai agita andu othe moke merire.

Mubango wa Gatandatu

## JESU KUHINGIA MUBANGO WA NGAI

**Muoroto wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kiririkaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Jerimia 31: 31-34

**Muhari Wa Kwiririkania:**

"Atiriri, matuku nimagoka maria ngarikanira kirikaniro kieru na nyumba ya Isiraeli, o na nyumba ya Juda". Jeremia 31:31

**MUTONGORIA:**

Thoma Afilipi 2:5-8; Mathayo 16:24-25. Hindi iria Jesu aciarirwo kirikaniro kia Iburahimu gikihinga. Ngai arikaniire na Iburahimu ati kuhitukira ruciaro ruake nduriri cithe niikarathimwo. Mathayo na Luka maheanite mutaratara wa njiarwa na njiarwa cia Kristo kwonania ati Jesu ni wa ruciaro rwa Iburahimu.

**GICUNJI KIA MBERE:** Kirikaniro Gikuru

Ciana cia Isiraeli niciaremirwo ni gutwara ndumiriri ya Ngai kuri thi yothe ta uria Ngai endete meke. Thoma Kiambiriria 26:4- 5. Riu Ngai atumagira ruciaro o rwa Iburahimu kurathima thi yothe.

Thiini wa muturire wa Jesu, Ngai nionanirie wendo wake nja ya thingo cia andu a bururi wa Isiraeli.

**GICUNJI GIA KERI:** Kirikaniro Kieru

Hindi iria Ngai atumire muriu thiini wa thi, athondeke kirikaniro kieru na andu eru. Aisiraeli matiacokire hindi ingi gutuika andu amure a Ngai. Andu amure a Ngai niaria mamukirite Jesu ta muhonokia na kwambiriria guthii na ngwataniro na Jesu.

Thoma Aroma 9:8. Yugaga,"...ati ti ciana iria njiare na muciarire wa mwiri ingituika cia Ngai, no riri, ciana iria cia kiiraniro, nicio cia gutuwo mbeu iria ya ma".

**GICUNJI GIA GATATU:** Jesu, Muhonokia wa Thi

Thoma Mathayo 13:31-33. Jesu agerekanirie uthamaki wa iguru na mbeu ya muthabibu ikiritwo mugate-ini.

Thoma Mathayo 5:13-o16. Tuthomaga uhoro wa ndumiriri ya mwathani kirima-ini. Jesu akira arutwo ake ati mahana ta cumbi wa thi na utheri wa thi. Ndumiriri ya mwathani Jesu ibataire gutuika utheri thiini wa nduma ya thi. Jesu arutire gakundi kanini ka andu nigetha mahunjie thi yothe uhoro-uria-mwega kuri andu othe a thi.

**MUTONGORIA:**

Kirikaniro Gikuru kuri ciana cia Isiraeli kigimainie na uhoti wa ciana cia Isiraeli gwathikira watho uria waneanitwo kuri Musa. Maathani ikumi mandikitwo ihengere-ini cia mahiga.

Kirikaniro kieru kiari ati watho wa Ngai ukorwo uri thiini wa andu. Akiandika mathani make ngoro-ini cia andu. Hindi iria Jesu oka thiini wa ngoro na muturire wa mundu, kirikaniro kieru no kuhinga kihingaga.

Mubango wa Mugwanja

## JESU NA AYAHUNDI

**Muoroto Wa Ithoma:** Ndumiriri Ya Kirikaniro Kuri Andu Othe

**Maandiko Matheru:** Luka 4:16-30

**Muhari Wa Kwiririkania:**
"Ni gukorwo Kristo niwe kirigiriro kia uhoro wa watho hari mundu o wothe witikitie, agatumaga atuwo muthingu." Aroma 10:4

**MUTONGORIA:**

Jesu ambiriirie kuhunjia na gutuma atumwo ake mbere kuri ciana cia Isiraeli. Ciana cia Isiraeli niciahetwo kanya kangi merire, metikie Ngai,mamwathikire na mahingie kirikaniro giake. Umu wa ngoro ciao ndwametikiririe metikie Jesu. Aisiraeli nimanyararite Ngai o na gukurwo meciragia ati o maari ahoi Ngai a ma.